ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tatu - Tarehe 03 Machi, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya MaaDILI ya Viongozi wa Umma Nam 4 ya mwaka 2015.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 93

Fidia Kwa Wanaocheleweshewa Kuungiwa Umeme

Mhe. Jaku Hashim ayoub (kny. Mhe. Abdalla Maulid Diwani) – Aliuliza**:-**

Kabla ya hapo naomba nitoe pole kwa Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa msiba alioupata na siku zote safari yetu ni hiyo moja hatujui saa ngapi wala dakika gani, *"Ina lillahi waina ilayhi rajiuun"*

Kutokana na ahadi nyingi zinazotolewa na Shirika la Umeme Zanzibar kuhusu shughuli nzima ya kuungiwa umeme kwa siku 21 baada ya kufanya malipo ya kuunganishiwa umeme.

a) Je, Shirika litawajibika vipi kwa kushindwa kuunga umeme ndani ya muda waliouweka wenyewe wa siku 21.

b) Je, Shirika liko tayari kulipa fidia kwa wananchi walio wacheleweshea kuwaungia umeme.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti**,** Kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake nambari 93 kama ifuatavyo:-

a) Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme bado linaendelea kutumia muda wa ndani ya siku 21 baada ya kufanya malipo uliowekwa katika muongozo wa huduma kwa Wateja wa kuwaungia umeme kwa kazi isiyohitaji nguzo. Hata hivyo, kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa Shirika, baadhi ya wakati upatikanaji wa huduma hiyo hukawia kidogo. Aidha, wizara yangu itaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa shirika linatekeleza muongozo huo kwa wakati.

b) Kama nilivyoeleza katika majibu ya swali (a) kuwa ucheleweshaji huo unatokana na sababu zilizo nje ya uwezo, hivyo haitokuwa busara kwa shirika kubebeshwa jukumu la kulipa fidia. Ni vyema ikafahamika kuwa madhumuni ya kuweka muongozo wa huduma zake kwa wananchi na kwa hivyo inapotokea mwananchi kuchelewa kupata huduma hiyo ieleweke kuwa ni tatizo la muda tu na sio dhamira ya shirika.

Mhe. Jaku Hashim ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi alisema hata hivyo, kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa shirika.

(a) Hebu atueleze sababu gani kama angalau tatu tu zilizokuwa nje ya uwezo. Maana kuna mengine tunaamini yamo ndani ya uwezo.

Nilimuuliza Mhe. Waziri hapa akakulinda kwenye swali la msingi watu wa Paje wamechukuwa karibu miezi sita na risiti zao nikazileta hapa kwa uthibitisho, hebu tueleze angalau sababu tatu wananchi wapate kufahamu.

(b) Kuna sababu ya hizi nguzo zinachukuwa muda gani kwenda kuondoshwa hasa katika eneo la Jambiani na kwengine ikiwemo Jangombe vile vile.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri jibu swali namba moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, hii inatokana na kwamba kufika kwa vifaa kama tunavyojua kwamba vifaa vyetu tunakuwa tunaagizishia. Kwa hivyo, inatokezea wakati vifaa hivi havifiki kwa wakati hiyo ni sababu kubwa na ya msingi ambayo inapelekea kuchelewa kidogo kwa uungaji wa umeme. Ahsante .

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kifungu 37 sijui utaniruhusu nikisome au kitakuwa kimeshafahamika kwa sababu naona maarufu humu ndani kifungu hichi sasa kwa mawaziri.

Mhe. Mwenyekiti: Sijakusikia bado sogea kwenye *mike*.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nasema nimesimama kuhusu utaratibu kifungu cha 37 sijui utaniruhusu nikisome maana yake kimekuwa maarufu sasa hivi ndani kwa *back bencher*.

Mhe. Mwenyekiti: Kisome.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante. Waziri au Mjumbe yoyote anaeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kwa usahihi kwa ufupi, sipokuwa kwamba swali alililoliuza waziri moja linaweza kujibiwa na waziri mwengine.

Nilimwambia anambie angalau sababu tatu alinambia moja tu na *hansard* zipo nilimwambia anambie sababu tatu hizi wananchi wapate kufahamu. Aniongeze nyengine mbili nyengine Mhe. Mwenyekiti, za ziada pamoja na suala langu moja kulikataa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Waziri muongeze majibu kama unayo. Katika lile lile jibu la kwanza ndio tunalotaka ujibu kama una jibu zaidi ndio hivyo, sio ujibu suala la pili hapana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, majibu ni yale yale.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, sijafahamu bado mimi.

Mhe. Mwenyekiti: Katibu.

Nam. 31

Ukosefu Wa Mchanga kwa Ajili ya Ujenzi

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: (kny. Mhe. Abdalla Maulid Diwani) - Aliuliza**:-**

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti, ngoja, ngoja Mhe. Mwenyekiti, kiti kinayumba sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf nilishapata barua kwamba Mhe. Jaku Hashim Ayoub ndiye atakayemuulizia maswali yake.. Kwa hivyo, Mhe. Jaku Hashim Ayoub ndiye atakayeuliza maswali ya Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Mhe. Jaku Hashim Ayoub uliza swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana. Lakini utaratibu wa swali hili moja linaweza kuulizwa nyongeza na watu lakini umeruhusu upande mmoja tu Mhe. Mwenyekiti. Kwa hiyo, hicho kiti kidogo Mhe. Mwenyekiti kiangalie.

Swali linaweza kuulizwa la nyongeza na watu wawili ikiwa mwenyewe mwenye swali la msingi na watu wengine wa ziada wawili kwa mujibu wa kanuni zetu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sitaki kuingilia hayo maamuzi yako mimi nafuata muongozo wako wewe ndie bosi wangu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba serikali itoe majibu ya swali namba 31.

Nam. 31

Ukosefu wa Mchanga kwa ajili ya Ujenzi

Mhe. Jaku Hashim Ayuob: (kny. Mhe. Abdalla Maulid Diwani) - Aliuliza**:-**

Jitihada za wananchi kutengeneza nyumba bora zimeathiriwa sana na tatizo la upatikanaji wa rasilimali ya mchanga ambao ndio nyenzo kubwa katika ujenzi huo na kupelekea usumbufu wa upatikanaji wake.

Je, Wizara yako inatoa tamko gani kuhusu kadhia hii ya kukosekana mchanga.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani wa Jimbo la Jang'ombe swali lake nambari 31 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu imeingia katika changamoto ya upungufu wa rasilimali ya mchanga kwa kadiri ya wiki tatu hivi. Kadhia hii ya upungufu wa mchanga imetokana na kuthibitika kwa taarifa za utafiti ulianza kufanyika tokea mwaka 2015. Kiwango cha mchanga uliopo nchini umepungua sana isipokuwa katika maeneo ya kilimo, vianzio vya maji na makaazi ya watu ambayo ni maeneo hatari kimazingira na kijamii ikiwa yataruhusiwa kuchimbwa mchanga basi yanaweza kuleta athari katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa imeundwa Kamati ya pamoja wizara tatu Wizara ya Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati, Maji, Nishati na Mazingira na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kuendelea kufanya utafiti wa kina ili serikali iwe na taarifa za kutosha za kufanya maamuzi juu ya nja mbadala za ujenzi zitakazothibitishwa kwa mujibu ya mazingira ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, utafiti juu ya namna bora ya kukabiliana na hali hii kwa sasa wizara bado haina tamko lolote Waheshimiwa Wawakilishi tunaombwa kuwa na subira hadi pale tutakapokamilisha utafiti huu. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, hili swali nafikiri ni la muda mrefu na sijui niseme wizara imekurupuka tu na maamuzi haya nilisema mtoto kwanza haachishwi maziwa siku hiyo ukisha kumnyonesha inachukuwa muda. Ilikuwaje maamuzi haya mkayatoa bila kuchukuwa maoni kwa wananchi na wananchi ndio walioweka serikali hii madarakani na bila ya wananchi serikali isingekuwepo.

Kwa nini msingetoa elimu hiyo kwa wananchi ili kuwaelimisha tumeshuhudia mifano mbali mbali kutokea maradhi ya miripuko ya kipindupindu wananchi wetu wanaelimishwa.

(a) Ni sababu gani za msingi mlizokuwa hamkuzitoa elimu ya kutosha kwa wananchi.

(b) Serikali inahitaji mapato ili na sisi tupate kulipwa mishahara yetu na maposho yetu, hivi sasa nondo hazitoki, matofali hayafanyiki, hali ya uchumi imezidi kuzorota, unatoa kauli gani Mhe. Naibu Waziri kwa hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri jibu swali namba moja kwa sababu yeye anauliza maswali mawili. Kwa hivyo, jibu swali moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, elimu inatolewa, imetolewa na itaendelea kutolewa kuhusiana na suala hili la mazingira au uharibifu wa mazingiram ambayo yanachimbwa mchanga.

Vile vile serikali ndio inategemea mapato lakini serikali haitegemei mapato hayo tu. Haiko tayari serikali kupokeo mapato halafu huku nchi yake ikawa inaharibika kimazingira. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi kama nilivyosema tusubiri utafiti unalizike siku hizi hizi za karibuni tutatoa bei za mchanga itakuwa iko vile vile na haitowaathiri wananchi wetu. Nashukuru.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasii, Mifugo na Uvuvi naomba kuuliza swali la nyongeza. Wananchi wa Zanzibar kwa asilimia 90 ni wanyonge na unyonge wao mtu akianza kujenga leo mwezi wa tatu 2017 ana miaka kumi siku nyengine kidogo kidogo ili amalize ujenzi wake kutokana na umasikini wetu.

(a) Je, kwa kuwa suala hili ni zito na kwa Zanzibar yetu tunaamini mchanga unachukuliwa upande mmoja wa Kaskazini tu.

(b) Serikali katika utafiti wao haijaona pahala pengine pa dharura kwa muda likatokea eneo kama Kusini mfano tu huo au Kati pahali ambapo pana mchanga unafaa ili tunusuru yale mazingira yalioko huku lakini huku watu wapate huduma ya mchanga.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli utafiti kama nilivyosema tena tusubirini tusiwe na haraka siku hizi hizi mbili tatu basi tutatoa taarifa na mchanga utaendelea kuchimbwa kama kawaida. Lakini kwa taratibu maalum ambazo serikali itakuwa imezipangia. Nashukuru.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana na ya ufasaha kabisa katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wawakilishi wanakumbuka kabisa kwamba serikali imeshatoa tamko kwamba rasilimali iliyobaki ya mchanga ni tani laki nne na nusu mahitaji halisi ni tani milioni moja na laki tisa. Kwa hivyo, serikali

lazima ichukuwe hatua hasa tukizingatia kwamba eneo peke yake ambalo lina mchanga linaloweza kutumika ni Mkoa wa Kaskazini Unguja na juzi tulikuwa Tume ya Mipango inawasilisha taarifa ya *house budget survey* imeonekana kabisa Mkoa wa Kaskazini umasikini unaongezeka na sababu kubwa ya umasikini kuongezeka watu wamebadilisha matumizi ya ardhi kutoka kilimo kwenda kuchimba mchanga hekta mia tano na sitini zimechimbwa mchanga matokeo yake hakuna kinacholimwa tena katika Mkoa wa Kaskazini.

Kwa hiyo, serikali chini ya uongozi wa Mhe. Dkt Ali Mohd Shein ambaye mwenyewe kwanza ana falsafa kubwa sana ya kiutafiti akasema hebu kwanza hili jambo tulizuie tuhakikishe kabisa hii rasilimali iliyopo ni vipi tunaweza kuitumia kwa uchache uliopo na hatimae tutoe jambo la mbadala ambalo litasaidia katika nchi. Nategemea Makamu wa Rais atakapofanya majumuisho ya shughuli zetu leo atakuwa ametoa kauli ambayo itatusaidia katika jambo hili. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kuuliza swali la ziada lenye (a) na (b). Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba utafiti umeanza karibu miaka 15 nyuma ana sehemu zozote ambazo zilizofanyika utafiti ambazo tayari zinakuwa na majibu.

(a) Kwa nini mpaka hii leo Wizara yake wameshakubali kwamba utafiti umefanyika hapo kipindi cha nyuma hawana majibu hadi lieo.

(b) Kwa kuwa suala la mchanga ni jambo sugu sana ambalo tumeshahisi kwamba Zanzibar itafika wakati itakuwa hakuna mchanga. Sasa watueleze mchanga mwengine utakuja kutoa sehemu gani baada ya hapa Zanzibar ili kuhakikisha kwamba mchanga utakuwa rahisi na hauna usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

(a) Mhe. Mwenyekiti, sikusema utafiti umefanyika nyuma isipokuwa tunafanya utafiti mbadala wa mchanga si kama mchanga utakuwa hautumiki utatumika lakini utakuwa matumizi yake mchanga ni asilimia ndogo sana ya matumizi yake.

(b) Mchanga upo kama alivyosema Mhe. Waziri lakini tani zilizokuwepo ni kidogo. Kwa hivyo, tunajitahidi kudhibiti isiwe wanachukuwa wachache halafu wengine wakakosa na zaidi wananchi wetu. Kwa hivyo, naomba tusubiri tumalize siku mbili tatu hizi litatoka tamko la bei na kila kitu kama

ilipanda bei basi bei itabakia pale pale mtu anaweza kuunza *minimum* lakini sio *maximum* ya ile bei ambayo serikali imesema. Nashukuru.

Nam. 36

Tatizo la Mmong'onyoko wa Ardhi

Mhe. Dkt Makame Ali Ussi - Aliuliza**:**

Kwa kuwa usafiri wa kwenda na kurudi katika sehemu zilizotenganishwa na bahari unaweza kurahisishwa kwa kutanua eneo la ardhi kwa kufukiya bahari na kujenga miundombunu inayostahiki.

(a) Je Wizara yako ina mpango gani unaolenga kurahisisha usafiri wa kwenda na kurudi katika sehemu zilizotenganishwa na bahari kwa masafa mafupi ambamo bado vinatumika vyombo vya baharini vinavyotumia muda mrefu.

(b) Je, Wizara yako haioni haja ya kuanza kufikiria utaratibu wa kufukia sehemu zilizokwisha kuvamiwa na bahari kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika kwa kujenga miundo mbinu husika ili kurahisisha usafiri katika sehemu hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi wa Jimbo la Mtopepo swali lake Nambari 36 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu ina mpango wa kutafuta boti za mashine *fiber boats* kwa ajili ya kuwasafirisha wananchi ambao wapo katika sehemu zilizotenganishwa na bahari.

Mhe. Mwenyekiti**,** boti za aina hii zilikuwepo hapo zamani na zilikuwa zikitoa huduma katika maeneo mbali mbali ya aina hii kama vile Chwaka, Marumbi n.k.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kwa hivi sasa haioni haja ya kuwa na utaratibu wa kufukia bahari kwa hivi sasa, kwani utaratibu huo unahitaji utaalamu mkubwa na vile vile kuna athari zake kimazingira. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Dk. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa jibu lake nusu zuri. Kwa kuwa tunaweza tukatatua tatizo la usafiri baharini, kwa mfano kwenye kisiwa chetu cha Tumbatu pale kwa kufukia baadhi ya sehemu baadae tukajenga kidaraja kidogo watu wakawa wanaingia na kutoka hata kwa miguu, inawezekana kabisa na nchi nyingi zimefanya hivyo.

(a) Kwa nini wasiandae utaratibu kama huo.
(b) Kusema kwamba haoni haja ya kufukia hilo ni tatizo, ni nchi nyingi sasa hivi zinafukia bahari ili kuongeza maeneo, wanajenga majumba, wanalima na kadhali. Sisi tukisema hatuoni haja, namuuliza Mhe. Naibu Waziri haoni kwamba tunajiweka nyuma na maendeleo ya dunia.
(c) Swali la tatu

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, usiongeze maswali mama,

Mhe. Dk. Makame Ali Ussi: aah! sio swali mama,

Mhe. Mwenyekiti: Swali la nyongeza ni (a) (b) na (c),

Mhe. Dk. Makame Ali Ussi: ni (a) (b) na (c),

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, mawili umeshauliza.

Mhe. Dk. Makame Ali Ussi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Kwanza napenda kumtoa wasi wasi Mhe. Mjumbe, sisi huwa hatujibu maswali nusu nusu wala hatutoi majibu nusu nusu. Huu ni mpango wa serikali na tunapojibu hapa tunajibu kwa uhakika kabisa.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi, sana akiwa ni rafiki yangu, kwamba tunapojibu maswali tunajibu kwa mujibu kwa vipaumbele vyetu na utaratibu wa ilani yetu ya uchaguzi na mambo mengine ya *Vision 2020*.

Kwa hivyo, nikiendelea kumjibu maswali yake nilimwambia kwamba kwa hivi sasa sio kwamba hatujaiona hiyo haja, lakini kwa hivi sasa kutokana na majukumu makubwa tulionayo na tuna vipaumbele vingi, tunamuomba sana

Mhe. Mjumbe atufahamu kwamba hayo ni mambo ya baadae. Wenzetu kweli wanafanya lakini ni gharama kubwa na serikali yetu hivi sasa ina vipaumbele vyake kwa mujibu wa ilani ya uchaguzi ya CCM, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam 82

Taratibu na Sheria za Usafiri wa Magari

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Ruhusa za madereva na magari ikimaanisha leseni na ruhusa nyengine kama beji hutolewa na kukaguliwa na Wizara ya Mawasiliano kupitia Idara ya Leseni. Baada ya kutoa na kukagua leseni hizo, Idara hiyo haihusiki tena na Sheria zake husimamiwa na Polisi kwa asiimia 100% na kesi ikiondoka hapo hupelekwa Mahakamani bila kushirikishwa kwa Idara hiyo.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa suala la magari na madereva baada ya kukamatwa kupelekwa Idara ya Leseni na wao ndio wakaandaa kesi na kuipeleka Mahakamani badala ya Polisi kusimamia masuala hayo kwa asilimia 100%.

(b) Je, Serikali haioni tatizo kutoa leseni na ukaguzi wa vyombo vya usafiri huku ikitokea ajali au uvunjaji wa Sheria ya masuala hayo ikasimamiwa na Polisi badala ya idara husika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said wa Jimbo la Chake Chake Mwakilishi swali lake nambari 82 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kupitia Idara ya Usafiri na Leseni hutoa leseni za madereva na huvikagua vyombo vya moto vinavyotembea barabarani.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa serikali haioni umuhimu wa suala la magari na madereva baada ya kukamatwa kupelekwa Idara ya Usafiri na Leseni kwa sababu, makosa yote ya usalama barabarani ni miongoni mwa makosa ya jinai. Utaratibu wa makosa ya jinai ni kwamba, Polisi baada ya kukamata anapeleleza na baadae kupeleka

kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ambae huipeleka kesi hiyo Mahakamani. Idara ya Usafiri na Leseni huwa ni Shahidi tu katika makosa hayo.

(b) Mhe. Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa serikali haioni tatizo kutoa leseni na kufanya ukaguzi wa vyombo vya usafiri inapotokezea ajali au uvunjaji wa sheria, masuala hayo yakasimamiwa na Polisi badala ya Idara, kwa sababu inapotokezea ajali, kunakuwa na mashirikiano kati ya Polisi na Idara ya Usafiri na Leseni katika kutafuta chanzo cha ajali hiyo. Chombo kilichopata ajali na leseni ya mhusika hukaguliwa na Idara ya Usafiri na Leseni. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Niongezee tu kwamba katika nchi za wenzetu sasa hivi hakuna tena utaratibu wa askari kumkamata mtu na kuanza kumpeleka mahakamani na kuanza kuhangaishana, *just* ni kumwandikia faini ya hapo kwa hapo au faini zile zikenda moja kwa moja katika leseni yake ambayo anaitumia.

(a) Je, ni lini utaratibu huu utaanza ili kupunguza matatizo haya kwa Zanzibar.

(b) Mara nyingi sana askari wanakaa barabarani kuangalia magari katika ubovu wake na ubora wake, wakati suala hili limewekwa kwenye sehemu ya mawasiliano na usafirishaji. Kwa nini askari wetu ambao wanakwenda kwenye maeneo ya ukaguzi hawachukui mtu ambaye anatoka mawasiliano au *Vehicle Inspector.*

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba hili suala la kufanya *notification* maana yake saini za hapo kwa hapo tumeliona na tumeshaanza kufanya utaratibu, ili baadae utaratibu huo kwa kupitia kanuni zetu ukiwa tutatangaza rasmi ni lini utaanza kutumika.

(b) Polisi sio kazi yao kukagua vyombo vinavyokuwepo barabarani, bali wao huangalia kile chombo na *road licence* na Bima na vile vile kutaka kujua leseni ya dereva. Sisi tunachofanya wakati wa ukaguzi ni kuwashirikisha wenzetu mfano Jeshi la Polisi na *ZRB* ili kufanya ukaguzi wa kupata kujua kama kile chombo kweli kimefaa kuingia barabarani, leseni ya muhusika Bima

na *road licence*. Kwa hivyo, hapo ndio tunaposhirikiana na polisi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nitauliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kwenye Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

(a) Kwa kuwa nchi nyingi wizara kama yako inaweka *speed limit* kwa waendesha magari haya ya abiria, wageni na kufika kuwafungia *engine*, ndani ya *engine* unaweka mashine fulani kwamba ikifika *speed 80*, inakuwa haiwezi kwenda zaidi ya *speed limit 80*.

Sasa kutokana na masuala ya ajali tulizokuwa nazo ndani ya Zanzibar kwa wingi ni lini sasa daladala na wanaopeleka wageni watu wa utalii gari zao utawafungia *speed limit* ambayo hawatoweza kwenda zaidi ya *speed 80* njiani.

(b) Zanzibar tumeona kuna magari mengi machakavu yanasababisha kutoa moshi hata yule mtu aliyekuwepo nyuma anakuwa haoni mbele kwa moshi ulivyokua mwingi.

Je, ni lini sasa utazifungia gari zote au zikatengenezwe mpaka ziwe sawa ambazo zinasababisha moshi mkubwa sana na kuharibu mazingira kwenye barabara.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama unavyojua masuala ya kufunga *speed governor*, ni masuala ambayo yanataka utaratibu maalum na kufanyiwa uchambuzi yakinifu.

(a) Kwa hivi sasa hata wenzetu waliokuwa wakifunga *speed governor* imeonekana kwamba madereva wanawachezea. Mimi bado nitahimiza kwamba tuendelee kutoa elimu na madereva wetu wawe waadilifu katika kuzifuata sheria zetu. Kwani wao pekee ndio wanaotakiwa kujua kwamba mwendo kasi unasababisha ajali na vile vile kupelekea vifo.

Kwa hivyo, mimi nawaomba sana madereva kwa kupitia Baraza lako tukufu, kwamba waendelee kuzifuata sheria zetu kwa mujibu tulivyozipanga.

(b) Aliuliza kwamba uchafuzi wa mazingira kwa gari zinazotoa *carbon*. Kama tunavyosema, sisi kila mwaka tunakagua gari na pale kunapokuwa na ukaguzi ule ambao tunaufanya basi sisi huangalia zaidi ubovu wa gari na hatarishi isisababishe ajali. Hili ni suala ambalo liko mazingira, lakini uchafuzi

wa mazingira hata sisi tunaupiga vita. Kwa hivyo, tutahimiza kwamba gari tuendelee kuziweka katika hali ya usalama zaidi kwa kuzifanyia matengenezo ya kila wakati. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh (Diaspora): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Mwenyekiti, kumetokea utaratibu Zanzibar wa *plate number* kuzibidua na zimeanza kutumika kwa njia mbali mbali kama ya uhalifu na ujambazi. Je, hii ni sheria, sera au utaratibu wa serikali umekubalika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, hiyo sio sheria na pale ambapo wataonekana madereva wanafanya jambo hilo, basi hatua kali zitachukuliwa dhidi yao. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 22

Huduma ya Bima ya Afya kwa Hospitali za Serikali Pemba

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa wananchi wamehamasika na wamekuwa wakijiunga kwa wingi katika mifuko ya Bima ya Afya ambayo tunaamini ina faida kubwa hasa kwa wananchi wa kipato cha chini. Hata hivyo kwa upande wa wananchi wa Pemba kumekuwa na usumbufu wa upatikanaji wa huduma za afya kwa kutumia Bima ya Afya hasa kwa hospitali za Serikali.

(a) Je, huduma ya Bima ya Afya inatumika katika vituo vingapi huko Pemba.

(b) Kwa nini Serikali isiimarishe utaratibu wa kutoa huduma za afya kwa kutumia Bima ya Afya katika hospitali zake za Abdalla Mzee, Chake Chake na Wete wakati huduma hii inaonekana kuimarika zaidi katika vituo vya watu binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake swali lake Nam. 22 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba wananchi wengi wa Zanzibar wamehamasika na kujiunga na mifuko ya Bima ya Afya.

(a) Huduma ya Bima ya Afya inatumika katika vituo 6 huko Pemba.
(b) Huduma hii pia iko katika hospitali zetu za serikali, yaani Wete, Chake Chake, Mkoani na pia kwa Micheweni iko katika kukamilisha utaratibu wa kuanza kutumia huduma hii. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na pia nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Mhe. Mwenyekiti, Bima ni mtu kitu ambacho anajihakikishia asilimia labda 50 kwamba utibabu wake atafanikiwa.

Kwa kule Pemba mara nyingi unaweza ukaenda kutaka matibabu au kutaka dawa, dawa zile zikawa hazipatikani ni lazima usafiri. Je, kwa sababu umeshamuahidi kumpa matibabu pale, Mhe. Naibu Waziri anamuhakikishia mgonjwa yule kwamba atapata tiketi ya kwenda kufuata sehemu ambayo atapata matibabu yale.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, huduma hii Pemba kwa hospitali za *private* pamoja na *public* kidogo ilichelewa kuhamasika, uhamasishaji wake ulikuwa mdogo. Kwa hivyo, hata wale watendaji wanaohudumia huduma hii afya ya Bima basi walikuwa hawajawa vizuri, zile taratibu kwa kweli walikuwa hawazijui vizuri sijui niseme, au elimu ilikuwa ni ndogo.

Lakini kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, nakuomba utembelee kwenye vituo hivi ambavyo vinatoa huduma hii, wako vizuri na mara nyingi dawa zinapatikana vizuri. Tatizo jengine kubwa nafikiri ilikuwa hawa watu wa Bima wenyewe, uwasilishaji wao katika vile vitengo pengine ulikuwa haujakaa, mipango yao ilikuwa haiko vizuri. Kwa sasa utaratibu uko vizuri, naomba utembelee na unieleza kama kuna matatizo ili niweze kufuatilia.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, nilikuwa nataka kujua ni mifuko ipi ya afya ambayo hospitali ya Mnazi Mmoja inakubalika. Kwa sababu kumekuwa kuna usumbufu kwa wagonjwa ambao wanatumia Bima ya *NHIF* wamekuwa wakisumbuliwa sana katika hospitali hiyo kwa kuambiwa kwamba Bima yao haikubaliki. Je, ni mifuko ipi ambayo hospitali ya Mnazi Mmoja inakubalika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mifuko ambayo inakubalika au inatumika katika hospitali zetu zote ni huu wa *Private Health Insurance*, lakini hata hii *National Health Insurance Fund* pia huwa inakubalika kwa baadhi ya hospitali. Sina uhakika wa asilimia mia moja kwamba pale wanatumia mifuko hii yote mimili au wanatumia zaidi huu mfuko wa *Private Health Insurance*, hilo sijawa na uhakika zaidi. Lakini najua mifuko hii yote miwili tunaitumia katika hospitali zetu za serikali.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona na kwa kuuona upande wako wa kushoto. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo lenye (a) na (b) ya nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kwuwa Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein alikuwa akipigania kwa nguvu zote, kuwezesha Bima ya afya ya taifa Zanzibar ili iwe nayo moja kutumia pesa zetu za ndani.

(a) Je, ni sababu zipi mpaka leo hatujaweza kuanzisha Bima hiyo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, *ZSSF* ni moja ya mifuko imara na mikubwa zaidi hapa Zanzibar, kwa nini sasa tusiishawishi kuweza kuweka mfumo wa Bima ya Afya ya Taifa kwa kupitia *ZSSF*.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na ninamshukuru sana Mhe. NaibuWaziri wa Afya kwa majibu yake mazuri kabisa.

Kwanza kabisa hivi sasa kwa kauli ya Mhe. Rais mwenyewe aliyoitoa na aliirudia tena mnamo tarehe 01 Mei, pale alipokuwa anaazimisha siku ya wafanyakazi duniani, kwamba huu mfuko utaanzishwa na mfuko huu pia umo katika ilani ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2015/2020. Kwa hivyo, mchakato wa kuanzisha mfuko huu unaendelea serikalini, na hivi sasa tumeshafikia hatua nzuri sana na tayari tumeshawahusisha wale wanaoitwa wadau au wahusika wakuu, ili kutoa maoni yao na ile sheria iweze kuendelea mbele zaidi katika vikao husika. Hilo la kwanza.

Lakini la pili namuomba Mhe. Dimwa aelewe kwamba sera ya *Afro Shirazy Party* na Sera ya Chama cha Mapinduzi, ambayo imerithi kutoka *Afro Shirazy Party*, ni kumpatia mwananchi wa kawaida matibabu bila ya malipo. Mfuko huo utakaoanzishwa utakuwa unawagusa zaidi wale waliokuwa katika sekta rasmi, yaani walioajiriwa, kwa sababu waajiri wao watachangia. Lakini naomba pia nimuhakikishie kwamba tunashirikiana kwa karibu sana na *ZSSF* katika mfuko huo ambao unatakiwa kuanzishwa na kuna mjumbe mmoja

ambaye ni mjumbe wa kudumu katika hiyo *Steering Committee*, kamati ya kuanzisha mfuko huo, yuko mjumbe mwengine kutoka Utumishi wa Umma, yuko mjumbe mwengine kutoka *Private Sector* wote hao wamo katika ile kamati, yaani *Steering Committee* ya kuanzisha mfuko huu.

Kwa hivyo, namuomba nimuhakikishie, kwa sababu ya sera yetu ya Chama cha Mapinduzi, na sera ambayo tumeridhi ya *Afro Shirazy* ya kutoa matibabu bila ya malipo kwa wananchi, tunatarajia mfuko huu utakapoanzishwa uta-*cover* wale watu ambao wanafanyakazi. Lakini wananchi wengine wote wataendelea kupata matibabu bila ya malipo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 100

Kukamilishwa Jengo la Huduma ya Upasuaji Micheweni

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondoa)

Utaratibu

Mhe. Mwenyekiti: Sema utaratibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante. Mhe. Mwenyekiti, katika *order paper* hii ya leo, nilizungumza jana Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kilio cha mchanga na ufutaji wa ardhi, nikaahidiwa labda serikali italeta kauli. Lakini bado muda haujesha naendelea kuhimiza tu, kuna msemo unasema shika shika na mwenyewe uko nyuma, na mimi ndio nahimiza hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naam.

Mhe. Mwenyekiti: Sikusikii vizuri, tumia vizuri *microphone* ili niweze kukusikia nini unachokizungumza. Umesema utaratibu sema utaratibu uliokusudia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Nilikuwa nina ahadi yangu hapa leo hii kabla Baraza halijafungwa kuhusu kauli ya serikali, kuhusu tatizo la upatikanaji mchanga na serikali iliahidi kwamba itatoa kauli, na shughuli inamalizika leo. Pia kuhusu ufutaji wa viwanja. Nilisema huwezi kujenga kiwanja bila ya kuwa na mchanga, nikaahidiwa leo. Nashukuru serikali ipo, lakini bado sijapata jawabu mpaka muda huu tokea tarehe 15/02/2017 hadi

hivi sasa na leo Ijumaa tunategemea kumaliza Baraza. Nasubiri kwa hamu kauli ya serikali kuhusu suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe Jaku hilo suala litazungumzwa wakati wake ukifika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, samahani wakati wake ukifika hii leo.

Mhe. Mwenyekiti: Waziri wa Kilimo ameshaeleza kwamba jawabu itapatikana kwa hivyo tusubiri Waziri nae anajiandaa na suala hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kwa heshima kabisa yale yalikuwa ni masuala na majibu sio kauli, ni masuala na majibu sasa kama tunaanza kuyumbisha kiti Mheshimiwa tokea jana kiti kinayumba.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Serikali ipo inakusikia na jawabu ipo itapatikana.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii ningependa nimtanabahishe Mhe. Jaku kwamba Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali alitoa ufafanuzi kwa kina juu ya suala linalohusu mchanga, lakini vile vile Mhe. Waziri alitoa maelezo mazuri kwenye suala hilo. Lakini pia kuna *Hansard* ya tarehe 23/2/2017 katika Baraza lako hili tukufu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Kilimo alielezea kwa ufasaha sana juu ya maelezo ambayo Mhe. Jaku anataka ufafanuzi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba Serikali imesema jambo hili inazidi kulifanyia kazi na serikali inaelewa kwamba rasilimali ya mchanga ni sekta kubwa sana, sekta inayogusa shughuli za kijamii na za kiuchumi katika nchi yetu, inaelewa fika umuhimu wake na manufaa yake kwa wananchi na dhamira kwamba mchanga huo utumike vizuri kwa maslahi ya watu wetu na taifa letu kwa sisi tuliokuwepo leo na vizazi vinavyokuja. Lakini pamoja na kuhakikisha kwamba zile athari za kimazingira zinazotokea kutokana na uchimbaji huo wa mchanga zinaondoka, nia ya Serikali ni matumizi mazuri ya mchanga huu kwa utaratibu mzuri, imeamua Serikali kufuaitia kwa karibu zaidi kuhusu rasilimali hii ya mchanga na tumesema hapa katika hotuba ya ufungaji ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ataelezea suala hili kwa kina zaidi.

Kwa hivyo ningemuomba ndugu yangu Mhe. Jaku akavuta subira sisi sote tuliopo hapa tunawatumikia wananchi nia yetu ni kuwatumikia vizuri wananchi wasipate athari, tunajua maumivu makubwa wanayopata wananchi wetu kwenye kusimama kwa muda kwenye suala hili la mchanga, tunaelewa fika kuujua umuhimu huu tunaujua ugumu huo lakini pia tunaangalia na upande wa pili wa athari ambazo zinatokea na zinazoweza kupeleka kuathirika sana nchi yetu. Kama tunavyojua hiki ni kisiwa tukiendelea kuchimba bila ya utaratibu maalum kinaweza pia kuingia maji bahari, kinaweza pia kuathirika kwa njia moja au nyengine kutokana na hali ya tabia ya nchi inayoendelea duniani kote kwa hivyo hatua zinazochukuliwa ni kuhakikisha kwamba matumizi hayo yawe salama kwetu sote kwa nchi na wananchi wake.

Naomba sana wananchi wetu watuelewe nia na dhamira njema ya Serikali juu yao na nawahakikishia kwamba kama alivyosema Naibu Waziri asubuhi hii kwamba leo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atatoa maelekezo vizuri na naamini kabisa kuanzia jumatatu utaratibu mzuri umewekwa wananchi watapata fursa hii ya kuendelea na kuchimba mchanga kama utaratibu utakavyowekwa na Serikali, utaratitu ulio mzuri na makini na baada ya hapo niseme tu kwamba hizi zitakuwa ni hatua za dharura ya kutatua tatizo lililo mbele yetu na bado Serikali inaendelea kufanya utafiti wa kina ili ije na ufumbuzi wa kudumu kwenye suala hili kubwa ambalo lina mahitaji yetu sote kwa sisi na vizazi vinavyokuja.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Jaku aendelee kusubiri ngojee hotuba ya Mhe. Makamo wa Pili na halafu atapata taarifa rasmi kupitia Wizara husika ya kilimo ikitoa ufafanuzi wa maelekezo kamili. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti: (*Makofi*)

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumshukuru Mhe. Mohammed Aboud kwa umakini wake na uhodari wake na niombe na Mawaziri wengine wajaribu kufuata nyayo zake, Mhe. Mohammed Aboud akikufahamisha kitu ukatulia hakurupuki na niwanasihi Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri maneno mazuri ni sadaka.

Mhe. Mohammed Aboud nimekufahamu sana lakini suala la asubuhi lilikuwa ni masuala na majibu na ahadi ya Serikali ikatoa kauli na *Hansard* nnazo kwa nia njema kabisa na leo siku ya Ijumaa. Suala la asubuhi ni la maswali na majibu sio kauli ya Serikali kama nilivyoahidi ipo hapa Hansard ……

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku kwa mimi nilivyomuelewa Mhe. Waziri ameshatoa ufafanuzi na jawabu itapatikana atakapokuja Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kwa hivyo ufafanuzi suala la mchanga linakuja naomba ukae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti…..

Mhe. Mwenyekiti: Naomba ukae ….

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ngoja hizi hoja zilikuwa mbili bado moja…

Mhe. Mwenyekiti: Naomba ukae Mhe. Jaku nakuomba ukae.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona kwa sababu najua pengine shingo yako inakuwa inakuuma hutizami huku mara kwa mara, lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka tuende kwenye Kanuni 43 Kiongozi wa Shughuli za Serikali au Waziri yoyote anaweza kutoa kauli katika Baraza kuhusu jambo lolote ambalo Serikali itawajibika. Na baada ya hapo Mwenyekiti wa kamati anayehusika au Wajumbe wengine anaidhinishwa na kamati anaweza kupewa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati juu ya kauli hiyo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti tuende 43(3) Hapatakuwepo na majadaliano yoyote kuhusu kauli yoyote itakayotolewa kwa mujibu wa kanuni hii, lakini Wajumbe wanaweza kwa idhini ya Spika, kumuuliza maswali Waziri aliyehusika na kauli hiyo kwa madhumuni ya kuelimishwa zaidi juu ya maelezo ya kauli hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku amezunguma kuhusu kauli ya Serikali na jana Mhe. Spika, ambae alikialia kiti hicho alisema Serikali itafanya utaratibu wa kutoa kauli juu ya jambo lile. Sasa tukiwa tunakwenda nje ya hivyo unavyosema Mhe. Mwenyekiti, wewe unahusika na kuvunja kanuni hizi za Baraza la Wawakilishi na kama nilivyozitaja. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, inapaswa Serikali ilete kauli ili tuiulize kufahamu zaidi tukawafahamishe wananchi weu. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kama nitasiklizwa kwa makini kuhusu niliyoeleza ni kwamba bado Serikali inalifanyia kazi kwa kina zaidi jambo hili, kwa sasa hizi zote ni hatua za dharura kwa hivyo pale mchakato mzima utakapomalizika ndio serikali inaweza kutoa kauli ya mwisho kwenye jambo hili na ikatoa nafasi kwa Waheshimiwa wajumbe kuuliza, bado tumo katika kutafakari, lakini kutokana na umuhimu wa rasilimali hii kubwa kwa wananchi wake ndio maana kumechukulil hatua kwa Serikali kuunda kamati maalum chini ya Makamu wa

Pili wa Rasi ulifuatilia kwa kina kujua undani na kuona kwa hatua hizi za dharura kulipatia ufumbuzi wa muda ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao bila ya usumbufu, ndio maana kuna maelekezo ambayo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atayatoa mbele ya Baraza hili tukufu.

Lakini bado wakati wetu kama serikali kutoa kauli rasmi ni baada ya mchakato mzima kufanyika kwa sababu bado utafiti unaendelea ili tuseme maneno yenye uzima katika jambo hili kubwa, Serikali haikurupuki wala haifanyi kazi kwa matakwa ya mtu inaanya kazi kwa mujbu kwa hivyio nataka niseme wazi bado msingi wetu wa kuja kuleta kauli ijadiliwe wakti ukifika tutafanya hivyo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na hoja yake nzuri sana, lakini kinachozungumzwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atakuja kutoa hotuba wakati akiahirisha baraza, na wananchi wale kupitia wawakilishi wao watakuwa hawawawezi tena kuhoji jambo lolote atakapokaa mbele.

Mhe. Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku kauliza suala zuri sana kwa manufaa ya watu wa ZAnzibar, na ikiwa tangu kipindi kile Serikali bado haiwezi kutoa tamko hapa sijui itatoa wapi.

Mhe. Mwenyekiti: Kwanza niwaombe wajumbe wote walioko nje ya ukumbi kama wapo mkahawani warudi na walipo ndani wasitoke kwa shughuli iliyoko mbele yetu, wajumbe wote ambao wako nje ya ukumbi kama wako Mkahawani warudi huku tunaendelea na kuweka sawa suala hili.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti kanuni hiyo hiyo ya 43 sisi tuliahidiwa leo kwamba itatoka kauli kwa mujibu wa maneno ya Mhe. Spika, sasa tukiambiwa kwamba bado kuna utafiti haujakamilika hiyo kauli itatoka vipi, sisi tunachotaka na naamini Serikali kama inasema Jumatatu itatoa kauli basi jibu wameshakuwa nalo *before.* Sasa bora hebu leo tupewe jibu kabla hajaja Makamu hapa kwa sababu akija Makamu sie tushafungwa hapa hatuna lolote la kuinuka na kauli itakuwa ishapigwa tikitaka tunaomba sana tuipate kauli kabla Mhe. Makamu wa Rais hajaja kuhutubia Baraza la kulifunga.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tusikilize taarifa kutoka kwa Mhe. Waziri kwa maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nawashukuru sana wajumbe kwa *concern* yao juu ya tatizo la mchanga ambalo wananchi wetu linawakabili, lakini kama alivyosema Mhe.

Mohammed Aboud Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba tarehe 23/2/2017 nilielezea utaratibu ambapo Serikali huwa inatoa kauli katika Baraza lako tukufu na nilisema kwamba ili Serikali itoe kauli katika Baraza lako tukufu ni lazima kauli hiyo ipitishwe na Baraza la Mapinduzi na si vyenginevyo halafu ndio kauli hapa inakuja. Kwa kuona hali halisi na tatizo lililopo tarehe 23 nikajaribu kuelezea hatua ambao Serikali imechukua na ambazo inaendelea kuchukua na hatimae kauli rasmi itatolewa.

Kwa kuwa utafiti bado haujakamilika nikaja nikatoa kauli tena hapa hapa barazani kwamba hatua za dharura zinachukuliwa baada ya hapo ndio kauli rasmi itachukuliwa ka sababu gani, mama nilivyoelezea hivi sasa kwamba tani za mchanga zilizopo ni laki nne na nusu, mahitaji ya wananchi kwa mwaka ni tani laki mbili na nusu, mahitaji ya kampuni binafsi ni tani laki milioni moja na laki nne. Kwa hivyo lazima Serikali ije na mpango makini kusema katika kipindi cha miaka mitatu mitano wananchi hawa rasilimali hii wataitumiaje na utafiti ni *prosess* unaweza ukafanya utafiti leo ukamaliza likazuka jambo jengine ukafanya tena utafiti, kwanza utafiti haumaliziki katika dunia. Jambo lile moja unafanya utafiti na unashtukia jambo jengine unafanya utafiti kwa hivyo hatua ya kwanza ambayo tumefanya ni kuondoa hili tatizo ambalo liko hivi sasa.

Kwa hivyo sio kauli ile ambayo inakwenda kwenye kina mpaka kusema miaka mitatu minne inakuwaje lakini katika hali ya dharura tunafanyaje, ndio Serikali ikasema Makamu wa Rais utakapofanya majumuisho nenda katoe kauli au taratibu wa hii hatua ya awali tunafanyaje baada ya hatua hiyo ndio tutakuja rasmi kwenye Baraza kutoa kauli, baada ya Baraza la Mapinduzi kuridhia utafiti ambao unafanywa utakapokamilika halafu utaletwa, lakini kwanza tuondoe shida ya wananchi iliyopo. Sote tuko *concerned* tunajua kama kuna tatizo. Hizi tani laki nne na nusu zilizopo tunazitumiaje kuondosha tatizo hili hadi hapo utafiti utakapomaliza kujua hasa katika kipindi cha miaka mitatu minne mitano tunafanyaje katika jambo hili.

Hilo ndilo tulilolieleza na na tumelieleza katika Baraza hili na *Hansard* hii hapa wakasome watu ipo, kwamba huo ndio utaratibu wa Serikali, Serikali haikurupuki na utafiti ni *prosses* sio kama unamaliza leo halafu kesho usifanye tena jambo jengine hilo ndio nililolizungumza. Kwa hivyo nawaomba sana Waheshimiwa tunaelewa *concern* yenu, tunaelewa kwamba kweli lakini nasema na Serikali iko makini sana katika jambo hili. Hii ni sekta ambayo ina-*involve* si chini ya watu laki moja na nusu, wako wanaochimba mchanga kule, wanaochukua mchanga, wanaotumia mchanga, wanaojenga n.k kuna miradi ya Serikali peke yake *Airport* hii hapa inataka tani laki mbili na nusu za mchanga,

Bakharesa anataka tani laki sita za mchanga tukimpa rasilimali tuliyokuwa nayo hivi sasa mchanga wote umemaliza unakwenda unakurupuka na kauli tu hivi kienyeji enyeji hapana, lazima utafute utafiti wa kina ujue kampuni za Serikali zitapataje tuna mashule chungu nzima yanataka mchanga.

Nina listi ya makampuni zaidi ya 38 kuna miradi ya kijamii hospitali sasa hamuwezi mukakurupuka tu kienyeji enyeji, lazima muende mahala museme Serikali itapata mchanga, makampuni binafsi yatapata mchanga na taasisi nyengine zitapata mchanga.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri nakuomba ukae kidogo.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Kwa sababu hiyo Mhe. Mwenyekiti, nakuomba sana tumalize hili jambo na mimi nakuambia kabisa Serikali iko makini katika hilo.

(Hapa Mhe. Spika, alikalia kiti)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nilikuwa namalizia tu kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi *concern* ya Serikali kwamba tuhitaji rasilimali hii tuitumie vizuri sana haipo ni chache tunafanyaje. Lakini kuna madhara mengine ambayo makubwa yanatokea katika nchi, nenda kaangalie maeneo ambayo yamechimbwa mchanga mimi naomba mpate fursa mwende mkayatembelee maji ya bahari yako karibu sana. Unapochimba mchanga unachimba mita tatu visiwa vyetu hapa hivi sasa level ilivyo watu wanakwenda wengine mpaka mita nne wanachimba. Kwa hivyo kuna *level* ya maji ya bahari vile vile yanaingia. Kwa hivyo Serikali lazima iwe *concered* sio kwa ambao tunachimba mchanga tu je, maisha ya binaadam yataendeleaje mbele ya safari kwa hivyio tunaweza kuzungumzia mchanga lakini kuna athari nyengine lazima tuziangalie.

Nawaomba sana wananchi nataka nimshukuru sana Mhe. Rais wetu ni mtu makini amepelekewa taarifa zaidi ya nne akasema hapana kafanye utafiti wa hichi, fanyeni hichi na hichi hakubali kukurupuka hata Kwa maana hiyo hiyo naomba sana tuvumilie hili jambo, yeye akisharidhika kwamba utafiti wetu umekamilika ndio tuje na kauli rasmi ya Serikali tukihakikisha kabisa utafiti umekamilika, tukielewa kwamba nchi yetu sasa inakuwa. Mimi nashukuru sana leo Wazanzibari wanataka kujenga maendeleo yanazidi kuongezeka mahitaji haya yatazidi kuongezeka. Sasa Serikali iliyo makini haipangi kwa siku mbili tatu inapanga kwa miaka mitano kumi na kumi na tano ndio utaratibu wetu wa mipango.

Nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wavumilie nawahakikishia kabisa Serikali ipo pamoja nao ipo pamoja na wananchi na jambo hili tutalipatia ufumbuzi wa haraka kwa muda mrefu, kwa muda wa kati na kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Utaratibu

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, ulipokuwa umeingia hapa kulikuwa kuna mgongano kidogo wa kauli zinazotoka humu ndani, kwamba Mhe. Jaku hoja yake alizungumzia alikuwa anataka kauli ya Serikali kuhusu suala zima la uchimbaji wa mchanga na uzuiwaji ulioko sasa hivi na hatua zitakazochukuliw. Kwa hivyo kupitia kwako Mhe. Spika, ukaelekeza kwamba Serikali itakuja na kauli. Sasa kwa mujibu wa kanuni zetu ambazo Mhe. Mohammed Said Mohammed *(Dimwa)* alivitaja hivyo vifungu vinazungumza kwamba kauli ya Serikali inatakiwa lazima Mwenyekiti wa Kamati aitolee maoni, lakini vile vile wajumbe wapewe nafasi ya kuuliza maswali.

Sasa hapa mgongano uliokuwepo kwamba Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili, yeye alisema kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atakapokuja kutoa hutuba yake atatoa hiyo kauli ya Serikali, sasa utaratibu wa Baraza hauko hivo kwa sababu hotuba ya Makamu wa pili wa Rais ya kufunga Baraza ile ni ya kuahirisha Baraza huwezi ukauliza suala. Hili Mhe. Spika, ili lisije likajirejea tena hata katika Baraza lililopita tuliambiwa hapa kuna kauli kuhusu masuala ya ng'ombe tukaambiwa kauli itatolewa na kwa bahati mbaya Mheshimiwa Spika, Serikali kauli zake inapitishia kwako halafu wewe ndo unatamka matokezeo yake tunakuona kama wewe ndio mkosa. Maana yake unasema Serikali italeta kauli, sasa kama Serikali haijaleta kauli ina maana kauli yako imekiukwa sasa mimi nilikuwa naomba tu muongozo wako tu Mhe. Spika, maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, hivi sasa maelezo yale kama angeleta kwa maandishi akayasoma ikawa kama kauli ya Serikali nafikiri ingekuwa nafasi tosha ikawacha Mwenyekiti wa Kamati akaitolea maoni na wajumbe wakauliza maswali. Halafu baadae kupitia yale masuala yatakayoulizwa huo utafiti unaoendelea kufanywa na maamuzi ya Serikali utapata vile vile *support* ya masuala yanayoulizwa waheshimiwa vyengine katika kuboresha utekelezaji huko baadae.

Lakini kwa sasa hivi hicho kitu kinaonesha kimeshakosekana sasa sijui kiti chako kitatumia busara gani, na hivi sasa hivi Makamu wa Pili anataka kufunga Baraza sasa kama labda ingekuwa Baraza linafungwa jioni mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri maelezo yake angeyaandaa akayaandika vizuri baadae

tukarudi akatoa kauli ikatolewa maoni tukauliza masuali halafu Makamu wa Pili wa Rais akafunga Baraza. Lakini vyenginevyo sasa hivi Hotuba ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais ile kwa mujibu wa Kanuni zetu siyo taarifa ya Serikali au sio kauli ya Serikali ambayo sisi tutaweza kuitia nyama. Mheshimiwa Mwenyekiti huo ndio mgongano ulokuwepo sasa tunaomba muongozo wao.*(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa Hamza nimekusikia na nimekuelewa Waheshimiwa Wajumbe tunajua hapa pana mambo mengi yamejizonga kwanza kabisa ni suala lenyewe hili la mchanga limekuwa ni la muhimu sote tunakubaliana ni suala muhimu sana. Lakini utaratibu wetu huku ndani tunaenda kwa mujibu wa vitu tulivyoviweka katika *order paper*. *(Makofi)*

Sitaki niruhusu mjadala kuhusiana na suala la mchanga sasa hivi kwa sababu katika *order paper* hatuna kitu hicho lakini kuna kitu muhimu tu suala la Serikali kwamba ingetoa kauli kuhusiana na hili suala la mchanga lakini pia tunafahamu kwamba tuna *hansard* ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aliowahi kutoa akalizungumzia suala hili lakini inaonekana bado Waheshimiwa hawakuridhika na kauli hiyo walioipata siku hiyo. Waheshimiwa Wajumbe, sikusudii kwamba tuahirishe jioni leo tutaahirisha hivi asubuhi lakini suala hili mimi ningeomba basi mara baada ya kuahirisha hili Baraza hapa, tukae Ofisi ya Baraza kwa maana ya Spika, Mheshimiwa Makamu wa Pili, Waheshimiwa ambao wanaguswa na kadhia hii, Mhe. Jaku, Mhe. Hamza na Mheshimiwa gani mwengine, sawa mimi nafikiri sote hatutoweza kukaa, tupate tu wawakilishi wachache, wenyeviti wa kamati tunaweza tukakaa kikao tukalitatua lakini wenyeviti hao pamoja na mwenye hoja Mhe. Jaku, Mhe. Jaku utakuwemo kwenye hiyo timu.

Tukae tulizungumze hili suali kwa sababu Serikali ipo tutakubaliana wakati huo nani na nani aingie tukae tulizungumze tulimalize. Lakini tuwache huu utaratibu wa Baraza uwende mpaka tumalize hizi shughuli kwa mujibu wa *order paper* ilivyopangwa. Mimi nadhani tunaweza tukafikia pahali kwa sababu kazi zenu waheshimiwa hamzifanyi Barazani tu mnazifanya Majimboni natunazifanya Maofisi humu kwa hiyo Kikao hicho tutakachokikaa kitakuwa ni sehemu ya shughuli hizi hizi. Mimi naomba tukubaliane hilo halafu tuendelee na hizi shughuli ambazo tunazo hapa lakini hatimae bila shaka tutaweza kufikia muafaka kuhusiana na suala hili la mchanga. Waheshimiwa Wajumbe, baada ya maelekezo yangu haya sasa naomba niwite Katibu kwa shughuli inayoendelea. Katibu.

Uchaguzi wa Mjumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mtakumbuka kwamba tuna shughuli inayohusu uchaguzi wa Mjumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi tulikwisha kuifanya kwenye *caucus* huko sasa inabidi taratibu zile za Kibaraza zifuatwe. Kuhusu kura, kuhusu nini Mheshimiwa.

Muongozo

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Kuhusu suala la mchanga ufafanuzi kidogo.

Mhe. Spika: Hapana Mheshimiwa tulikubaliana baada ya hapa tukutane. *(Makofi)*

Ahsante Waheshimiwa kama mtakumbuka kwa wale ambao tuliopiga kura kule kwenye *caucus* kwamba tulitoa jina la mtu mmoja Mhe. Rashid Makame Shamsi. Sasa mimi nitakachokifanya ni kumwita Mhe. Rashid Makame Shamsi aje ajieleze mbele yenu halafu tuhesabu idadi ya Wajumbe ambao wamo ukumbini ili tuweze kupiga kura na kulimaliza suala hili. Mhe. Rashid Makame Shamsi tafadhali.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika kwa kunita hapa kwa neno ambalo liko mbele yetu mimi ndie Mhe. Rashid Makame Shamsi, ambaye nimegombea nafasi ya Ukamishna katika Tume ya Bajeti ya Baraza niwaombe ndugu wajumbe mnipe kura zenu ili kuweza ku-*cover* nafasi hiyo na *inshaallah* nitaitumikia vyema. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Shamsi maswali kama Waheshimiwa mnayo, maswali.

Waheshimiwa Wajumbe: Hakuna.
Mhe. Spika: Samahani kuna swali moja. Mhe. Nadir.

Mhe. Nadir Abdul latif Yussuf: Mhe. Spika nakuomba kumuuliza swali moja tu Mhe. wangu makini Mhe. Jembe tunafahamu ni mtu mzuri sana wa mahesabu mtendaji makini na muadilifu je huko utakapokwenda kwenye masuala ya mahesabu uko *fit* kututetea mambo yetu.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika na nimshukuru sana muulizaji kwa kweli katika suala hili la Bajeti mimi kwanza *profession* ni

mwalimu halafu nimeshika nafasi mbali mbali ambazo zimenipa uzoefu sana katika masuala ya bajeti kwa hiyo sina wasiwasi katika kuimudu nafasi hii na imani inakuteteeni vyema katika maslahi yenu. Ahsante sana.*(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid unaweza ukamalizia nenda kakae. Mhe. Abdalla Ali Kombo una swali tena keshaondoka. *(Vicheko)*

Taratibu msimuangushe Mheshimiwa.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Kwanza namshukuru Mhe. Rashid kwa kufanikiwa kwa kura zote swali langu aaa kura kesha pata swali langu unakwenda kwenye Bajeti mambo ya pesa na mambo haya kuwafanya watu sana kuwa na jeuri kuna wenzako walikaa hapo pale tukawapigia kura saizi kutusemesha inakuwa mashaka wewe itakuwaje?*(Makofi)*

Mhe. Rashid Makame Shamis: Ahsante sana Mhe. Spika na nimshukuru sana Mhe. Abdalla kwa kutoa wasiwasi wake mimi nnaimani mtakapo nipa hiyo nafasi basi nitakuwa kama Mhe. Rashid kama kawaida. Kwa hivyo nitaendelea kuwa na mashirikiano mazuri na Wajumbe wote wa Baraza hili kama kawaida yangu. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Rashid. Katibu naomba hesabu ya wajumbe wa waliomo ndani.

Katibu:. Mhe. Kuna wajumbe 63.

Mhe. Spika: Ahsante naomba kura zigawiwe.

(Hapa Waheshimiwa waligaiwa karatasi za kupiga kura)

Mhe. Spika: Waheshimiwa wakati tunaendelea kupiga kura kwa kuwa mgombea mwenyewe alikuwa ni mmoja tu nilitamani sana niwahoji tu ili tupige kura ya kuhoji naomba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais ategue kanuni kwa sababu kwa mujibu wa kanuni kwa mujibu wa kanuni tupige kura ya siri sasa kutengua ili kwa kura hii tupige ya sauti tu ya kuhoji.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kabla ya kufanya kazi ulonituma ningependa sana nichukue fursa hii kumpongeza Ndugu Rashid Makame Shamis kwa kugombea nafasi hii ambayo mimi mwenyewe binafsi sina shaka kwamba ataweza kuifanya vizuri

ni mmoja katika wawakilishi makini sana katika Baraza hili anafanya kazi zake vizuri. *(Makofi).*

Kwa hivyo tuna kila sababu kutengua kanuni ya kura badala ya kupiga kura ya siri tupige kura ya dhahiri kutokana na umakini wake mkubwa, kwa hiyo kwa ruhusa yako naomba Baraza lako Tukufu tutengue Kanuni badala ya kupiga kura ya siri tupige kura ya dhahiri tuoneshe waheshimiwa wajumbe kwa wananchi wetu kama tuna watu wazuri wanaohitaji kufanya kazi katika Baraza lako Tukufu. Mhe. Spika naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na hoja hii ni ya kutengua Kanuni zetu kuhusiana na upigaji wa kura ya siri badala ya kupiga ya siri tupige kura ya dhahiri sasa hivi wale wote wanaounga mkono hoja hiyo wanyanyue mikono yao wanaokataa wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Baada ya hapo sassa naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana na Mhe. Rashid Makame Shamsi kuwa Mjumbe wa Bajeti wanyanyue mikono yao wanaokataa waliokubali wameshinda. Katibu kwa shughuli inayofuata.*(Makofi)*

HOJA YA SERIKALI

Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya Mwaka 2015

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Spika: Naomba sasa nimwite Mhe. Waziri Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa niaba yake Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora): Mhe. Spika kwa niaba ya Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora naomba kusema ifuatavyo:

Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya Mwaka 2015 kusomwa kwa mara ya kwanza. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Katibu kwa shughuli inayofuata.

Katibu: Mhe. Spika, shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano huu zimekamilika.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe. Kwa kuwa Shughuli zote zilizopangwa kwenye Mkutano huu zimekamilika, sasa naomba kuchukua nafasi hii kwa heshima kabisa kwanza kukupongezeni kwa namna ambavyo mmeshiriki na masuala mbali mbali tumeyafanya hapa tokea tumeanza Mkutano huu. Kwa hivyo, nachukua nafasi hii sasa kumkaribisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili aje awasilishe Hotuba yake ya ufungaji wa Baraza. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tafadhali sana. *(Makofi).*

KUAHIRISHA BARAZA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kufanikisha Mkutano wetu wa Tano wa Baraza la Tisa la Wawakilishi, ulioanza tarehe 15 Februari, 2017.

Aidha, tumshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa neema ya amani na utulivu aliyotujaalia tukaweza kushirikiana na wananchi kuijenga nchi yetu katika hali ya amani, utulivu na salama.

Mhe. Spika, katika Mkutano huu wa Tano (5) wa Baraza la Tisa (9) wajumbe wako waliuliza jumla ya maswali 106 ya Msingi na maswali ya nyongeza 269 Maswali yote haya yalipatiwa jawabu za kuridhisha na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wao.

Naomba kuchukuwa nafasi hii kuwapongeza kwa dhati Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujibu maswali hayo kwa usahihi.

Mhe. Spika, Baraza lako Tukufu pia lilipata fursa ya kujadili jumla ya Miswada Mitatu (3) ambayo hatimaye ilipitishwa kuwa Sheria. Miswada iliyowasilishwa ni kama ifuatayo:-

i. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Namba 9 ya mwaka 1992.

ii. Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Nembo Namba 1 ya mwaka 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Namba 12 ya mwaka 2004 na kutunga Sheria inayoweka masharti bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ya 2016 na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

iii. Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sheria namba 2 ya mwaka 2006.

Mhe Spika**,** Kupitishwa kwa Miswada yote hii na Wajumbe wako kunadhihirisha wazi hali ya kuwa na Sheria bora nchini katika masuala ya Uchaguzi, utumiaji wa Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar pamoja na masuala ya Chakula, Dawa na Vipodozi.

Nawaomba wale wote watakaopewa majukumu ya kuzisimamia Sheria hizi zitakapoanza kutumika kuwa waadilifu wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Nawaomba pia wananchi kujenga utamaduni wa kufuata sheria bila ya shuruti.

Mhe. Spika, Baraza lako pia lilipokea Ripoti saba (7) za Kamati za Kudumu za Baraza lako Tukufu. Ripoti hizo ni kama zifuatazo:-

i. Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2016/2017.
ii. Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2016/2017.
iii. Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2016/2017.
iv. Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2016/2017.
v. Ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya mwaka 2016/17.
vi. Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya mwaka 2016/2017.
vii. Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) ya mwaka 2016/2017.

Mhe. Spika**,** ripoti zote hizo zilizopitishwa zimetoa nafasi kwa Wajumbe wako kutoa maoni, michango na mapendekezo kwa uwazi. Kwa kuwa Serikali yenu ni sikivu, tunaahidi kuyafanyia kazi maoni hayo pamoja na ushauri na mapendekezo yaliyotolewa ili azma yetu ya kujenga ufanisi na uwajibikaji Serikalini ifikiwe. Nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia ripoti hizo. Nakiri kuwa ripoti hizo zimechangiwa vizuri sana. Lakini pia niwapongeze Wenyeviti wa Kamati zote kwa kuleta ripoti zilizochambuliwa vizuri sana. Nawaahidi Wenyeviti kuwa kazi yao nzuri waliyoifanya itapata majibu mazuri kutoka Serikalini hapo mwezi wa Septemba, 2017.

Mhe. Spika**,** katika Kikao chako hichi pia Waheshimiwa Wajumbe walileta Hoja Binafsi mbili (2) ambazo ni:

i. Hoja binafsi ya Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) inayohusu Madawa ya Kulevya

ii. Hoja Binafsi ya uimarishaji wa mfumo mzima wa Kisheria unaoshughulikia uendeshaji wa kesi za udhalilishaji wa Wanawake na Watoto, Zanzibar iliyowasilishwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa. *(Makofi)*

Napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe walioleta Hoja Binafsi hizo. Hoja hizo zina umuhimu mkubwa na ni za msingi. Serikali imezipokea, imezitolea maelezo na inaahidi kuzifanyia kazi. Hoja zote mbili zimeelezea mambo ambayo yanayotia aibu nchi yetu. Hivyo sote kwa ujumla wetu tushirikiane katika kuyapiga vita na hatimae yatoweke kabisa.

Mhe. Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikuja Barazani kuzungumza na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi baada ya sisi wenyewe kumuomba kwa muda mrefu kuja kuzungumza nasi..

Jambo la kusikitisha ni kuona kwamba mitandao ya kijamii ilijazwa propaganda zisizokuwa na mashiko ya kwamba, Mheshimiwa Rais, alikuja kuvunja Baraza eti amkabidhi Serikali Maalim Seif Shariff. Nawaomba wananchi na wana CCM kwa ujumla wasibabaishwe na wala wasihamanike na propaganda hizo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein itabaki kuwepo madarakani mpaka 2020. Maalim Seif hana ubavu wa kuwa Rais

wa Zanzibar kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na hata baada ya Uchaguzi huo maana hawezi kushinda hata siku moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Serikali iliyopo madarakani ni Serikali halali ya Chama Cha Mapinduzi iliyochaguliwa na wananchi inayoongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein. Serikali hii haitotoka mikononi mwa Chama Cha Mapinduzi watasema wasemavyo, watachoka lakini kazi bure tu labda waendelee kufurahisha mabaraza yao na nafsi zao. Wewe Mhe. Spika, utaendelea kuwa Spika, Wawakilishi tutaendelea kuwa Wawakilishi kwa rehema za Mungu na Mawaziri na viongozi wengine wataendelea kuwepo madarakani hadi hapo Mheshimiwa Rais atakapoamua vyenginevyo na sio kwa propaganda uchwara za Chama cha CUF. Hivyo, nawaomba viongozi wenzangu tuendelee na jukumu la kuwaletea maendeleo wananchi wetu kwani ndio kazi waliotuwekea hapa maana sisi tumeshawazoea tangu mwaka 1995 hayo hayo ndiyo yaliyokuwa maneno yao ya kudanganyana anaapishwa kesho, keshokutwa mtondogoo hadi sasa hakuna kitakachotokea wasubiri 2020.

Mhe. Spika, Mnamo tarehe 29 Januari, 2017, Serikali yetu kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ilitoa taarifa kwa vyombo vya habari juu ya uhaba wa maliasili ya mchanga inayoikumba Zanzibar. Taarifa hiyo ilifuatiwa na usitishaji wa muda wa uchimbaji wa mchanga nchini. Taarifa hii ilikuwa na nia ya kuweka utaratibu mzuri wa uvunaji wa rasilimali hiyo na wala haikuwa na nia ya kuwatesa wananchi.

Ukweli usiopingika ni kuwa nchi yetu inakabiliwa na uhaba mkubwa wa rasilimali ya mchanga. Kama hatukuweka utaratibu maalum hali itakuwa mbaya zaidi kwa kipindi kifupi kijacho. Kwa hatua za awali za kukabiliana na changamoto hii, Serikali imeunda Kamati ya Wataalamu na Kamati ya Mawaziri. Miongoni mwa kazi za kamati hizo, ni kuangalia ukubwa wa uharibifu huo na hatua za kuchukua, kuangalia mahitaji halisi ya mchanga, kuorodhesha maeneo yanayopatikana mchanga, kuweka usimamizi mzuri wa kuchota mchanga pamoja na namna ya kuyarejesha maeneo yaliyochimbwa mchanga katika hali yake ya kiasili.

Mhe. Spika, napenda kuwajulisha Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa jumla kuwa Kamati ya Wataalamu na Kamati ya Mawaziri inayoshughulikia suala la mchanga imetoa maamuzi yafuatayo:-

Kuanzia siku ya Jumatatu tarehe 06 Machi, 2017 Serikali itafungua rasmi mashimo ya kuchimba mchanga. Hata hivyo, Serikali inalazimika

kuchukua uamuzi mgumu wa kusimamia moja kwa moja uchimbaji wa mchanga badala ya wananchi, pamoja na kutoa bei elekezi ili kuzuia uharibifu wa mazingira na ulanguzi wa kupita kiasi kwa wauzaji wa mchanga.

Mhe. Spika**,** pamoja na hatua hizo Serikali inatoa utaratibu kuwa kuanzia sasa maeneo ya kilimo hayatoruhusiwa kuchimbwa mchanga. Wizara ya Kilimo itaandaa zamu za kuchimba mchanga ili kupunguza msongamano wa magari katika maeneo ya kuchimba mchanga, zamu hizo zitakuwa kwa wananchi wa kawaida kuchimba mchanga siku tatu (3) kwa wiki. Aidha, makampuni yenye vibali vya ujenzi pamoja na Taasisi za Serikali zitapangiwa siku mbili (2) kwa wiki. Siku za Jumamosi na Jumapili zitakuwa siku za mapumziko hakutakuwa na uchimbaji wa mchanga. Serikali itafanya utafiti wa kujua kiwango cha mchanga kiliopo kwenye maeneo ya Kiwanda cha Sukari Pangatupu, Kichwele na maeneo mengine ili kujua wingi wa mchanga uliopo na kama unafaa kwa matumizi ya ujenzi. Kazi hii itafanyika katika kipindi cha wiki moja kuanzia leo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pamoja na hatua hizo Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, Ardhi, Nishati na Mazingiza na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafiri zitaandaa muongozo wa uingizwaji wa bidhaa za ujenzi ikiwemo mchanga, kokoto, kifusi na Mawe kutoka nje ya Zanzibar. Aidha, Serikali itafuatilia utaratibu uliotumika katika uuzaji wa maeneo ya kilimo kwa ajili ya kuchimba mchanga ili kubaini kwa kina ujanja uliotumika kuyabadilisha matumizi ya maeneo ya kilimo na kudhibiti hali hiyo isiendelee. Vile vile, Serikali haitolazimika kulipa fidia kwa wamiliki wa maeneo yaliyoidhinishwa kuchimbwa mchanga itakapoamua kuchimbisha mchanga huo chini ya usimamizi wake, isipokuwa kwa mazao ya kilimo na mali zilizomo kwenye maeneo hayo.

Mhe. Spika, nawaomba Wawakilishi wenzangu tunaporudi Majimboni mwetu tuwaelimishe wananchi wetu juu ya uhaba wa mchanga unayoikabili visiwa vyetu. Pia nawashauri muwapangie wananchi wenu ziara maalum kwenda kuangalia hali halisi ya uhabirifu wa mazingira sehemu iliyochimbwa mchanga. Zanzibar si nchi ya kwanza kuwa na upungufu wa mchanga. Mifano ya uhaba wa mchanga imeshajitokeza katika nchi mbali mbali duniani zikiwemo Malaysia, Singapore, Phillipines na nyenginezo. Aidha, kuna ushahidi wa visiwa vilivyozama kutokana na kuchimbwa mchanga kupita kiasi, huko Phillipines visiwa vitano (5)

vimezama kabisa baada ya wimbi kubwa la uchimbaji mchanga ndani ya visiwa na maeneo ya fukwe yanayozunguka visiwa hivyo.

Mhe. Spika**,** udhibiti huu wa rasilimali ya mchanga unaweza kupelekea wananchi wetu wakavamia fukwe zetu kuchota mchanga, kwa hivyo, naziomba mamlaka zote nchini kupiga marufuku uchotaji wa mchanga kwenye fukwe ili tujiepushe na majanga na kuangamiza visiwa vyetu.

Mhe. Spika, Serikali itatoa adhabu kali kwa mtu yeyote atakaekwenda kinyume dhidi ya agizo hili la Serikali, kuhusu suala zima la uchimbaji wa mchanga. Pia Serikali itatoa adhabu kali kwa wenye magari ya punda, magari ya ng'ombe wanaochota mchanga katika maeneo yasiyoruhusiwa. Adhabu hiyo ikiwa na pamoja na kutaifishwa magari hayo ya punda na magari ya ng'ombe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi karibuni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli ametangaza rasmi vita vya Madawa ya Kulevya. Vita hivi ni kwa nchi nzima ikiwemo Zanzibar. Wale wanaodhani vita hivi ni kwa ajili ya Tanzania Bara peke yake tunawaeleza bayana kuwa wamepotea njia. Zanzibar haitakuwa kimbilio la waendelezaji wa biashara hii haramu ya Madawa ya Kulevya na badala yake itakuwa gereza lao.

Takwimu kutoka Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya zinaonyesha kwamba mwaka 2016 jumla ya kesi 37 ziliripotiwa kwenye Mahkama za Unguja na Pemba na ni mtu mmoja tu ndiye aliyetiwa hatiani. Kutokana na takwimu hizo inaonyesha kwamba ukubwa wa janga hili hauendani na kasi za kuwakamata wanaoingiza dawa za kulevya nchini na kuwapa adhabu stahiki.

Mhe. Spika, katika kudhibiti uingizaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya, Serikali imeunda Tume ya Uratibu wa Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Tume hiyo inafanya kazi kwa karibu na Jeshi la Polisi, pamoja na wananchi na vyombo vingine vya dola katika kuhakikisha kwamba janga hili la madawa ya kulevya nchini linamalizika kabisa. Jambo la muhimu ni ushirikiano wetu kwani watu hao wanaojihusisha na madawa ya kulevya tunaishi nao majumbani mwetu.

Mhe. Spika, Vita dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsi hasa kwa wanawake na watoto bado havijatoa matunda mazuri. Bado kuna ongezeko kubwa la vitendo hivi. Takwimu za mwaka jana kuanzia Julai

hadi Septemba 2016 jumla ya matukio ya udhalilishaji 218 yaliripotiwa Unguja na Pemba. Hali hii ni ya kutisha na inatoa ujumbe kuwa bado tunahitaji kushirikiana kwa karibu kutokomeza vitendo vya udhalilishaji nchini. Kila mmoja wetu awajibike kwa nafasi yake. Nampongeza Mhe. Asha Abdalla Mussa Mwakilishi wa Kiwengwa kwa kuleta Hoja Binafsi hii kuhusu jambo hili ambapo imetoa fursa kwa Wajumbe wote wa Baraza hili kutoa maoni yao. Maoni yote yaliyotolewa yameonyesha kuwa hili ni janga jingine nchini mwetu linalohitaji kupigwa vita kwa nguvu zetu zote.

Mhe. Spika, Kwa upande wa *TASAF*, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na hatua za utekelezaji wa mipango mbali mbali ili kuwawezesha wananchi kupiga hatua za kimaendeleo, kujiongezea kipato na kupunguza umaskini. Miongoni mwa mipango hiyo ni mpango wa Kunusuru Kaya Maskini - *TASAF* Awamu ya Tatu ambapo walengwa kutoka Shehia 204 za Unguja na Pemba wananufaika na Mpango huu. Aidha, katika kipindi cha Januari – April, 2017 wananchi kutoka Shehia 182 (104 Unguja na 78 Pemba) wanaendelea kunufaika na utekelezaji wa Miradi ya Kutoa Ajira za Muda katika maeneo yao kupitia Mpango wa *TASAF* Awamu ya Tatu. Miradi hiyo imejikita zaidi katika Sekta za Mazingira, Misitu na Umwagiliaji.

Mhe. Spika, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuendelea kushirikiana na Watendaji wa *TASAF* pamoja na wananchi hasa walengwa wa Mpango huu katika kuisimamia miradi iliyomo katika Majimbo yao na kuhakikisha fedha zilizotengwa zinatumika kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru wale wote waliotuwezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu wa Tano wa Baraza la Tisa la Wawakilishi kwa ufanisi mkubwa. Pongezi hizo zaidi ziwafikie watendaji wote wa Baraza hili la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu wa Baraza.

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza kwa dhati Wawakilishi wanawake kwa namna walivyochangia hoja mbali mbali zilizoletwa mbele ya mkutano huu. Wamechangia kwa umahiri mkubwa na kujiamini. Hii inaonyesha namna gani semina za UWAWAZA ilivyofanyakazi iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, Kwa kumalizia hotuba yangu, napenda kukupongeza wewe Mhe. Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti kwa kuliendesha vyema Baraza hili. Hekima na busara zenu zimesaidia sana katika kuumaliza mkutano huu salama. Pia nawapongeza Wakalimani wetu wa lugha ya

alama kwa kazi yao nzuri. Nawapongeza pia Wanahabari kwa kufanya kazi zao vizuri bila ya kuchoka katika kipindi chote tulichokuwa Barazani hapa. Kalamu zenu zimewawezesha wananchi wetu kufuatilia kwa karibu mijadala yetu. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wawakilishi wote na Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa mashirikiano yenu mliyonipa. Nawatakia mafanikio mema katika kutekeleza wajibu wenu kwenye Majimbo yenu. Lakini napenda niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe kwamba tutakaporejea hapa katika mkutano ujao wa Baraza letu Tukufu *Inshaallah* tusisahau kufuata Kanuni za Baraza ambazo tumezitunga sisi wenyewe. Kubishana na kiti hakuleti tija ila kunapelekea ishara mbaya kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kwa heshima na taadhima kutoa hoja kwamba, Baraza lako Tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumatano tarehe 10 Mei, 2017, saa 3.00 barabara za asubuhi panapo majaaliwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa nawaomba niwahoji wale wote waliokubaliana na hoja ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwamba tuahirishe mpaka siku ya Jumatano tarehe 10 Mei, 2017 wanyanyuwe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kuna tangazo Mnadhimu wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokea CCM anawataka Waheshimiwa wote wajumbe wa CCM wabakie humu ukumbini mara baada ya kuahirishwa Baraza. Tangazo moja tu.

Baada ya Tangazo hilo sasa Waheshimiwa Wajumbe naomba tusimame kwa ajili ya wimbo wa Taifa.

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wimbo wa Taifa uliimbwa kuashiria kumaliza kwa Mkutano)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa nachukua nafasi hii kutangaza kuwa naahirisha Baraza la Wawakilishi mpaka siku ya Jumatano tarehe 10 Mei, 2017 saa 3:00 barabara za asubuhi panapo majaaliwa

(Saa 4.45 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 10/05/2017 saa 3.00 asubuhi)